JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SIMU: 0715 20 31 88
0786203188/0657523301

SHULE YA SEKONDARI USAGARA,

P.O.BOX 330,

TANGA.

Kwa kujibu tafadhali rejea,

KUMB.NA.USS/9/4/ JUNE 2022

JINA LA MWANAFUNZI ..... MCHEPUO .....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI USAGARA TANGA 2022

1.0 UTANGULIZI:

1.1 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (V) katika Shule ya Sekondari Usagara mkondo wa **PCB/PCM/CBG/HKL/KFC/KEC**.

Shule ipo Tanga Mjini, ukifika kituo cha mabasi **KANGE** panda **DALADALA** hadi kituo kidogo cha mabasi kilichopo Tanga Mjini. Shule ipo takribani **KM 2.5** toka kituo kidogo cha mabasi ya mjini kuelekea mashariki. Kwa teksi si zaidi ya shilingi elfu tano **(5000/=)** kulingana na maelewano, au unaweza pia kutumia Bajaji au Bodaboda nauli isiyozidi **(2000/=)**.

1.2 Unatakiwa kuripoti shuleni siku ya jumapili tarehe **13.06.2022** kuanzia saa **2:00**asubuhi hadi saa **11:00** jioni, ukija baada ya saa **11:00** jioni ofisi itakua imefungwa, hivyo hutapokelewa. Hakikisha umekamilisha malipo yote kabla ya kufika shuleni nakusoma kwa makini fomu yote ili usikiuke maagizo.

Mwanafunzi awapo shuleni atakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii, pamoja na kufuata sheria zote za shule.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE:

(i) Mashati **mawili (2)** meupe ya mikono mifupi na yasiyobana.
(ii) Suruali **mbili (2)** za rangi ya ugoro zenye marinda **mawili** na zisizobana sh. **18,000/=** kila moja jumla sh. **36,000/=** tu. **(Zinapatikana shuleni kuepuka utofauti wa rangi ya kitambaa)**.
(iii) Viatu vya ngozi, rangi **nyeusi**, vya kufunga kamba **(sio buti)**.
(iv) Soksi **nyeupe** pea mbili.
(v) Sandals za ngozi zenye mikanda rangi ya brown **(sio za kuchomeka)** na ndala za kuogea.

Edit with WPS Office

(vi) Vesti nyeupe zisizopungua pea **nne (4). (Vesti za rangi haziruhusiwi).**

(vii) Ikiwa utahitaji kuvaa sweta, liwe la rangi ya ugoro **(brown)** la mikono mirefu, shingo ya **"V"** linapatikana Shuleni kwa sh. **20,000/=** tu.

(viii) Mkanda rangi **nyeusi** au **ugoro** usio na urembo na wenye buckle iliyo wazi katikati.

(ix) Tshirt **(2)** za michezo rangi ya **kijani kibichi** zisizo na maandishi au picha yoyote.

(x) Track suit na bukta za michezo rangi ya **Kijani kibichi** mbili.

(xi) Viatu vya michezo (**raba**).

(xii) Shuka **2** za rangi ya **blue** zinapatikana shuleni kwa sh. **9000/=** moja, jumla **18,000/=**

(xiii) Utalipa shilingi elfu arobaini (**40,000)** kwa miaka miwili (2) kwa kutumia **GODORO** la shule. (Huruhusiwi kuja na godoro lako)

Mzazi/Mlezi zingatia maelezo ambayo yametolewa hapo juu.

- **Siku ya kuripoti mwanafunzi aje akiwa amevaa track suit AU t-shirt ya michezo kama alivyoagizwa, viatu vya darasani vya ngozi au raba za michezo na si vinginevyo.** Nguo nyingine za nyumbani kama Jinzi, buti, t-shirt za nyumbani, kofia na nyinginezo **HAZIRUHUSIWI KABISA SHULENI** hata wakati wa kuripoti.

Pia mwanafunzi aje na:-

- Nakala 1 ya **CHETI CHA KUZALIWA.**
- Nakala ya **RESULT SLIP.**
- Picha 3 (**PASSPORT SIZE**) zenye **BACKGROUND BLUE** apige akiwa na shati jeupe.

-MWANAFUNZI ALIYEBAIDLISHIWA SHULE KUJA USAGARA AJE NA NAKALA YA KURASA YA MTANDAONI AMBAYO JINA LAKE LIPO KWA AJILI YA UHAKIKI
-MWANAFUNZI AJE NA BIMA YAKE KWAAJILI YA MATIBABU

2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE:

NA.	MCHANGO	KIASI	NAMBA YA AKAUNTI YA KULIPIA	JINA LA AKAUNTI
1	ADA	70,000/=	NMB - BANK 41701200074	HEADMASTER USAGARA S.S
	MICHANGO			
1	TAALUMA	20,000/=		
2	ULINZI	20,000/=		
3	UPISHI	20,000/=		
4	TAHADHARI	20,000/=		
5	SAMANI	15,000/=		
6	UKARABATI	15,000/=		
	JUMLA	**110,000/=**		
1	KITAMBULISHO	6000/=	LIPIA SHULENI	
2	T-SHIRT	12,000/=		
3	NEMBO 2 @ 3000	6,000/=		
	JUMLA	**22,000/=**		
1	BUNDA LA KARATASI (REAM 1, A4)		OFISI YA MAKAMU MKUU WA SHULE	

Edit with WPS Office

ZINGATIA:

- ❖ Malipo ya kulipia Akaunti ya **NMB**
- ❖ Malipo ya kulipia **Shuleni**
- ❖ Shule itapokea **"Original Bank Slip"** tu kwa malipo ya benki na sio fedha taslimu
- ❖ Malipo yote yafanyike kuanzia **Julai 01 2021 na kuendele** ili yaingie kwenye BAJETI ya MWAKA husika wa fedha.

2.3 MWANAFUNZI AJE NA VIFAA VIFUATAVYO:-

1. (a) Kwa mkondo wa PCM aje **SOFT BROOM** na **JEMBE** moja (1) lenye mpini.
   (b) Kwa mkondo wa CBG aje **SOFT BROOM** na **SQUEEZER** moja (1) lenye mpini.
   (c) Kwa mkondo wa PCB aje **SOFT BROOM** na **REKI** moja (1) yenye mpini.
   (d) Kwa mkondo wa HKL aje **HARD BROOM** na **KWANJA** moja (1).
   (e) Kwa mkondo wa KFC aje na **SET YA MOP NA NDOO YAKE** moja (1).
   (f) Kwa mkondo wa KEC aje **HARD BROOM** na **KWANJA** moja (1).
2. Sanduku la bati lisilo zidi mita moja **(Masanduku mengine hayaruhusiwi).**
3. Mto na foronya mbili za rangi ya **blue maasai**.
5. Chandarua kimoja rangi nyeupe.
6. Kijiko, kikombe, bakuli na sahani kwa ajili chakula.
7. Ndoo moja ya plastic.
8. Sandals na Ndala pea1.
9. Taulo ya kotoni 1.

2.4 MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI YA KITAALUMA.

Ili mwanafunzi aweze kusoma vizuri nakufanikiwa anashauriwa aje na vitu vifuatavyo kwaajili ya matumizi yake binafsi;

i. Advanced learners dictionary. (Oxford /Longman) – Kwa wanafunzi wa **HKL** na **KEC.**
ii. Kitabu cha General Studies **"Understanding GENERAL STUDIES for Advanced Level"**. 4th edition. By Joannes Bigirwamungu and Sospeter M. Deogratias. **Kwa wanafunzi wote.**
iii. Calculator fx. 991 – Kwa wanafunzi wa PCM, PCB na CBG.
iv. Stop watch (za kawaida za plastiki, digital) – Kwa wanafunzi wa PCM, PCB na CBG.
v. Dissecting kit – Kwa wanafunziwa PCB na CBG.
vi. Steppler – Kwa wanafunzi wote.

3.0 FOMU ZA KUAMBATANISHA NA BARUA HII:

USS III: -Fomu ya mwanafunzi kukubali kufuata sheria za shule. Fomu hii irudishwe shuleni ikiwa imejazwa siku ya kuripoti.

USS IV: - Hati ya Mzazi/Mlezi kukubali masharti ya shule. Fomu hii Ijazwe na kurudishwa shuleni siku ya kuripoti.

USS VII: -Fomu hii ipelekwe kwa Mganga Mkuu hospitali inayotambulika na serikali ili ampime mwanafunzi kisha irudishwe shuleni ikiwa imejazwa siku ya kuripoti.

.....
SINGANO, Z.
MKUU WA SHULE

Edit with WPS Office

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

USAGARA SHULE YA SEKONDARI,
S.L.P. 330,
TANGA.

Kumb Na. USS/9/4 TAREHE: .....

Mwanafunzi.....
S.L.P.....
.....

PICHA YA MWANAFUNZI

FOMU YA MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi ..... nakubaliana na sheria nataratibu zilizoorodheshwa hapa chini kipindi chote nitakapokuwa nasoma shuleni Usagara:
Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Na inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo **la lazima.**
(b) Mahudhurio **kamilifu** katika kila shughuli ndani na nje ya shule.
(c) Kutimiza kwamakini maandalio ya jioni (**Preparation**).
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa. **Viatu, sweta, soksi au jaketi lisilo sare ya Shule vitachukuliwa na havitarudishwa.**
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(h) Kila mwanafunzi awe na begi la shule"**School Bag**" rangi nyeusi au blue.
(i) Shule haitoi chakula maalum (**Special diet**).
(j) Shule hii ni ya serikali na serikali haina dini, Hivyo mwanafunzi anatakiwakutokujihusisha au kushawishi wengine kujihusisha na mambo ya imaniyanayoweza kuhatarisha **usalama** wa shule na jamii kwa ujumla. **Ibadanamambo yote ya kiimani** yatafanyika katika nyumba za ibada nje ya shulekulingana na ratiba ya shule. **Shule haina ulezi wa vikundi vya kiimani.**

3.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi.
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocane, mirungi, kubeli, ugoro, sigara n.k.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuoa.
9. Kusababisha mimba.
10. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi.
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

Edit with WPS Office

13. Kuruka fensi ya shule.
14. Kumiliki, kukutwa au kutumia **simu ya mkononi**.

Sahihi ya Mwanafunzi…… Tarehe……..

Sahihi ya dole gumba



……

HATI YA MZAZI KUKUBALI MASHARTI YA SHULE

Mimi ……
Mzazi/Mlezi wa ……nimesoma na kuyakubali masharti yote ya mwanangu kujiunga na Shule ya Sekondari Usagara. Pia nitasimamia utekelezaji wa sheria za shule alizopewa. Najua pia kuwa kumiliki simu, utoro na uchelewaji shuleni **HAVIKUBALIKI**.

Saini yaMzazi/Mlezi ……
AnuaniyaMzazi/Mlezi ……
Nambayasimuya Mzazi/Mlezi ……..…….

PICHA YA MZAZI/MLEZI

DOLE GUMBA

JINA LA MTAA: ----------
JINA LA MTENDAJI WA MTAA:----------
NAMBA YA SIMU: ---------- SAINI ----------
JINA LA KATA: ----------
JINA LA MTENDAJI KATA: ----------
NAMBA YA SIMU: ----------
SAINI: ----------

MHURI

****

FOMU USS VII

USAGARA SECONDARY SCHOOL,

Edit with WPS Office

P.O.BOX. 330,
TANGA.

MEDICAL EXAMINATION FORM

PART A

To Medical Officer,
.....
.....
.....

MR/MISS.....(Name in full)
Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time schooling course. The examinations should include the following categories (I-II) each category or sub-category of which will render the applicant in-eligible in case of a defect.

I. (a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal Diseases(s)
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
II. Neurosis
III. Other serious disease

Signature.....

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named and consider that he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time school course.

I. (a) Eye-Sigh.....
(b) Hearing.....
(c) Limbs.....
(d) Speech.....
(e) Venereal Diseases.....
(f) Leprosy.....
(g) Epilepsy.....

II. Neurosis
III. Other serious disease

Station..... Signature.....
Designation..... Date.....

Edit with WPS Office